Nuru ya Kiswahili, Juzuu 4(1), Juni 2025:86-114
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru41.86114

# Hotuba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere: Mwangwi wa Semi za Kiswahili

**Zuhura A. Badru**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**
zuhura.badru@udom.ac.tz

**Ikisiri**

Makala hii inahusu namna hotuba za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kuanzia hapa na kuendelea, atatajwa kama Mwalimu) zinavyoakisi semi za Kiswahili. Mwalimu ni Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika, na baadaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hotuba zake zinahusu mambo aliyoyapa umuhimu kama vile uwajibikaji, uhuru, umoja, bidii katika kazi, uhusiano wa kimataifa, siasa ya ujamaa na kujitegemea, elimu, pamoja na malezi. Data zilizotumiwa katika makala hii zilikusanywa kutoka katika matini mbalimbali, zikiwamo hotuba, vitabu na kamusi za semi. Data hizo zilichambuliwa kwa njia ya uchambuzi matini. Kupitia hotuba hizo, imeonekana jinsi fasihi inavyoweza kuathiri namna ya mtu kufikiri, kunena, kutenda pamoja na kutazama hali ya maisha. Katika hotuba zake, semi za Kiswahili zimeakisiwa kwa namna mbili: ya moja kwa moja, ambapo anatumia semi kusisitiza jambo, na isiyo ya moja kwa moja, ambapo maudhui yake yanaoana moja kwa moja na semi za Kiswahili. Kwa jumla, kupitia namna zote mbili, imedhihirika kuwa kuna uhusiano kati ya fikra za Mwalimu na semi za Kiswahili. Hali hii inadhihirisha kuwa fasihi ni taaluma ambayo inagusa nyanja tofauti za maisha. Kwa hiyo, ni vema fasihi ifundishwe na kutafitiwa kwa kuhusianishwa na nyuga zingine zinazogusa maisha.

**Dhana za Msingi**: hotuba, semi, mwangwi

## Utangulizi

Semi ni kipera cha fasihi simulizi ambacho, aghalabu, huhusisha tungo fupifupi ambazo huzingatia idili na tajiriba za jamii fulani. Miongoni mwa

dhima za tungo hizi ni kuadilisha, kusisitiza ujumbe, kuonya, na kupamba lugha katika mazungumzo ya kila siku. Semi hizi huwa nyepesi kueleweka kwa wazungumzaji; hivyo, hata ujumbe unaokusudiwa kutolewa hueleweka kwa wepesi. Hii ni kwa sababu hutumia amali za jamii ya wazungumzaji husika (Akida, 1981; Bukenya, Gachanja, & Nandwa, 1997; Ndungo & Wafula, 1993; Wamitila, 2001; Mng'aruthi, 2008; Mulokozi, 2017).

Kupitia semi, hata mtu mgeni huweza kufahamu utamaduni na mawazo muhimu yanayoongoza na kutawala fikra za jamii fulani. Hii ni kwa sababu mfumo mzima wa jamii hiyo hufumbatwa na kuwasilishwa kupitia tungo hizo. Kwa sababu hii, semi ni tungo muhimu ambazo huakisi jumla ya maisha ya watu, imani zao, namna wanavyofikiri na namna wanavyoendesha maisha yao katika nyanja zote. Miongoni mwa mazingira ambamo semi hutumika ni katika hotuba. Makala hii inamakinikia namna hotuba mbalimbali za Mwalimu zinavyojitokeza kama mwangwi wa semi za Kiswahili.

Mwangwi ni mbinu ya kifasihi ambayo hutumika kurejelea sauti, maneno, sentensi, tabia za wahusika, dhana, motifu, picha au dhamira ambazo zinajirudia katika kazi mbalimbali za fasihi. Hii inamaanisha kuwa watunzi wa fasihi wa muhula mmoja huweza kuathiriwa na watunzi wa fasihi wa muhula uliopita (Colby, 1920; Hollander, 1981; Corcoran, 2001; Petrino, 2010; Anderson, 2017). Mbinu hii ya kifasihi huwa na dhima ya kujenga uhusiano baina ya kinachozungumziwa na kilichopo katika jamii, kuongeza ladha katika mazungumzo au maandishi na kusisitiza jambo. Vilevile, huchora picha inayoakisi hali ya usambamba uliopo kati ya ulimwengu wa kubuni na ulimwengu halisi.

Kuna uhusiano wa mlalo baina ya dunia halisi na dunia ya kubuni. Hii inamaanisha kuwa kinachoonekana katika kazi ya fasihi, aghalabu, huwa na kiwakilishi au kisawe chake katika dunia halisi. Hali hii huleta kile tunachoweza kukiita uhusiano mlalo baina ya dunia ya kifasihi na dunia halisi (Albrecht, 1954; Keerthika, 2018 na Alfarhan, 2024). Semi, kama kipera kimojawapo cha fasihi, hakiepuki kaida hii kwani, ijapokuwa hizi ni kauli za kubuni, kuna visawe vyake katika ulimwengu halisi. Kutokana na mtazamo huu, hotuba za Mwalimu zinajadiliwa kama mwangwi wa semi za Kiswahili.

## Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliozaa makala hii ulitumia Nadharia ya Utamaduni ambayo iliasisiwa na Raymond Williams (1963) na kuendelezwa na Richard Hoggart (1970 & 1998) na Mary Douglas (2014). Ijapokuwa nadharia hii iliibuka kutoka katika nyuga za Sosholojia na Anthlopolojia, kufikia katikati ya 21, ilikuwa ikitumika katika fasihi. Msingi wa nadharia hii ni kuchunguza namna utamaduni unavyojenga tabia ya mtu, mahusiano yake na watu wengine, namna yake ya kufikiri, pamoja na kunena.

Kwa upande wa fasihi, Nadharia ya Utamaduni hujikita katika kuchunguza uhusiano baina elementi za utamaduni, miundo ya kijamii na fasihi. Nadharia hii hujigeza kwenye msingi kuwa kuna kanuni za maisha, imani, miiko na thamani za jamii ambazo mwanadamu anatakiwa kuzifuata ili aweze kupata maisha bora na kuchangia maendeleo ya jamii yake. Haya yote huakisiwa kupitia fasihi ya jamii husika na jamii hiyo hupata nafasi ya kuelewa miundo yake kupitia ishara na masimulizi ya kifasihi. Kwa jumla, Nadharia ya Utamaduni inaangazia uhusiano baina ya utamaduni, uhusiano wa kijamii pamoja na fasihi (Williams, 1963 & 2006; Offermans; 2010;

Oswell, 2010; Payne & Barbera, 2010; Ryan, 2011; Douglas, 2014; Kavitha, 2023). Kwa kutumia mawazo ya nadharia hii, uhusiano baina ya hotuba za Mwalimu na semi za Kiswahili umejadiliwa.

**Methodolojia**

Hotuba zilizotumika kutoa data za makala hii zimepatikana kutoka matini tatu ambazo zina mkusanyiko wa hotuba mbalimbali za Mwalimu. Matini hizo ni *Freedom and Unity: Uhuru na Umoja: A Selection from Writings and Speeches 1952-65* (1966b), *Freedom and Socialism: A Selection from Writings and Speeches 1965-1967* (1968), na *Freedom and Development/Uhuru na Maendeleo: A Selection from Writings and Speeches 1968-1973* (1973). Matini hizo zina mkusanyiko wa hotuba kuhusu uhuru na umoja, uhuru na ujamaa pamoja na uhuru na maendeleo. Matini hizi ziliteuliwa kwa sababu zilikuwa na mkusanyiko wa hotuba nyingi mahali pamoja na zilipangwa katika mada kulingana na uhusiano wake. Hii ilimsaidia mtafiti kupata data za mada moja katika matini moja.

Aidha, zilitafitiwa hotuba tatu ambazo hazikuwa katika mkusanyiko. Hotuba hizo ni hotuba aliyoitoa tarehe 27 Agosti 1966 katika Chuo cha Ualimu Morogoro, hotuba aliyoitoa tarehe 4 Novemba 1985 katika Ukumbi wa Diamond Jubilee, na hotuba aliyoitoa tarehe 6 Machi 1997 jijini Accra. Hotuba hizi ziliteuliwa kwa sababu zilibeba mawazo ambayo hayakuakisiwa katika hotuba zilizokusanywa. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa mbinu ya uchambuzi matini.

**Uhusiano baina ya Hotuba za Mwalimu na Semi za Kiswahili**

Sehemu hii inajadili namna hotuba za Mwalimu zinavyohusiana na semi za Kiswahili. Mjadala huu umegawanywa katika vipengele sita. Msingi wa

vipengele hivyo ni maudhui yaliyobeba uzito katika hotuba za Mwalimu zilizotafitiwa. Vipengele hivyo ni tendo na tokeo, uhuru, umoja, uwajibikaji, kujitegemea, na malezi.

**Nukuu zenye mwangwi wa semi zinazohusiana na tendo na tokeo**

Dhima mojawapo ya semi ni kujenga na kuimarisha uwezo wa mtu kufikiri kwa kumfanya mtu huyo kuutazama ulimwengu wake kwa kina, huku akitambua namna watu wengine kwenye jamii wanavyoutazama ulimwengu waliomo. Aidha, semi hufanya mtu kutambua yaliyopita, kuiona hali ya sasa, na, hivyo, kumchochea kufikiria yale yanayoweza kutokea katika siku zinazofuata. Hii ni kutokana na kuwa semi hutumia lugha ya mafumbo na sitiari ambayo humlazimisha mtu kufikiri kwa makini kuhusu jambo linalozungumziwa. Vilevile, katika kufumbua mafumbo na sitiari hizo, mtu huona waziwazi namna ambavyo maneno na matendo huweza kuathiri maisha yake. Hili linaweza kuonekana dhahiri katika methali kama vile "Fikiri kabla ya kutenda" au "Haraka haraka haina baraka" ambazo husisitiza umuhimu wa kufikiri na kupima matokeo ya jambo kabla ya kulifanya. Hii ni kwa sababu mtu huweza kujutia uamuzi wake iwapo hakufikiri kwa makini hapo awali.

Mawazo ya namna hii yanathibitika katika hotuba ya Mwalimu anaposema: "*If you break a principle, it will find a method of breaking you. And if a people try to break a major principle those principles find a way of breaking that people*" (Nyerere, 1966:127). Mwalimu anamaanisha kuwa, "Ukivunja kanuni, nayo itatafuta mbinu ya kukuvunja na, watu wakijaribu kuvunja kanuni muhimu, kanuni hizo zitatafuta njia ya kuwavunja watu hao". Tafsiri hii na zote zinazofuata—zilizo sanjari na matini ya Kiingereza ya nukuu hizo—ni za mwandishi wa makala hii). Kauli hii inaonesha imani

ya Mwalimu kuwa hakuna tendo lisilokuwa na tokeo. Kwa hiyo, iwapo mtu atafanya tendo fulani, basi mtu huyo atarajie kuvuna jambo linalofanana na tendo lake. Mtazamo huu unaakisiwa na methali mbalimbali za Kiswahili. Miongoni mwazo ni "Hakuna masika yasiyo na mbu", "kila mchuma janga, hula na wa kwao", 'Mtenda hutendwa", "Aanguaye huanguliwa" na "Mcheza na tope humrukia". Katika methali hizi, kila jambo huambatana na tokeo lake. Aidha, kauli hii inaelekeza kuwa kila tendo la mwanadamu huitikiwa na jibu lake. Hii inamaanisha kuwa imempasa mtu kufikiri kila tendo na kila neno, kisha kupima kinachoweza kuzaliwa na tendo au neno tajwa.

Akiendelea kujadili jambo hili linalohusiana na tendo na tokeo lake, Nyerere (1966:22) anasema:

> *The only certain thing is that if we forget our principles, even when we are ignoring or breaking them, then we shall have betrayed the purpose of our revolution and Africa will fail to make its proper contribution to the development of man kind.*
>
> Jambo moja la uhakika ni kuwa tukisahau kanuni zetu, hata tunapozipuuza na kuzivunja, tunakuwa tunasaliti lengo la mapinduzi yetu na Afrika itashindwa kutoa mchango wake yakini kwa maendeleo ya mwanadamu.

Mwalimu aliamini kuwa kuna kanuni zinazotakiwa kuzingatiwa katika kuendesha maisha ya mtu. Kuzingatiwa kwa kanuni hizo ndiko humfanya mtu huyo kutoa mchango stahiki kwa maendeleo yake na hata jamii pana. Hivyo, iwapo kanuni hizo zitavunjwa, basi jamii husika isitarajie kufikia viwango vya maendeleo vinavyotarajiwa. Mawazo haya yanaweza kuhusianishwa na methali isemayo, "Mla mbuzi hulipa ng'ombe". Methali hii inaashiria kuwa, kabla ya mtu kutenda jambo ambalo, pengine, linaonekana dogo, akumbuke kuwa anaweza kupata matokeo kwa kiwango kikubwa. Ni kwa msingi huohuo, mataifa ya Afrika yanaonywa na

Mwalimu kuwa, iwapo kanuni za kiutu kama vile uhuru, heshima, haki, wajibu na kufanya kazi zitavunjwa, basi Afrika pamoja na ukubwa wake haitaweza kutoa mchango unaotarajiwa katika maendeleo ya mwanadamu.

Mwalimu anapojadili uhusiano wa tendo na tukio anaangazia suala la utamaduni wa Afrika katika muktadha wa ulimwengu. Anatambua kuwa Afrika haiwezi kujitenga na jamii zingine za kilimwengu. Hata hivyo, anaona kuwa kuna umuhimu wa kufikiri kwa makini namna bora ya kuhusiana na jamii hizo bila kutupilia mbali tamaduni ambazo zinaifanya Afrika kuwa bora. Anasema, "*A nation that refuses to learn from foreign culture is nothing but a nation of idiots and lunatics ... But to learn from other cultures does not mean we should abandon our own*" (Nyerere, 1966:187). Anamaanisha kuwa, "Taifa linalokataa kujifunza kutoka tamaduni za kigeni ni taifa la wajinga na vichaa … Lakini kujifunza kutoka tamaduni zingine hakumaanishi kuwa tutupilie mbali za kwetu." Nukuu hii inadhihirisha sifa mojawapo kubwa ya Mwalimu ambayo ni kuwa na fikra zenye mizani.

Mwalimu hakuwa mtu wa kuficha kichwa ndani ya mchanga na kujitia utando wa macho kutoona uhalisi wa maisha. Kila jambo aliliweka katika mizani, akalipima na kutafuta namna bora ya kulishughulikia ili kuleta athari chanya. Maudhui ya nukuu hiyo ya Mwalimu yanaakisi methali kama vile, "Usiache mbachao kwa msala upitao", "Usiteme jojo kwa karanga za kuonjeshwa", na "Mwenda tezi na omo marejeo ngamani". Methali hizi zote zinasisitiza kuwa mtu hapaswi kuyaendea kwa pupa au kibubusa mambo yanayohusu mabadiliko, bali ayaendee kwa umakini. Kwa muktadha wa nukuu za Mwalimu, maingiliano baina ya jamii moja na nyingine yana faida zake. Hata hivyo, jamii inatakiwa kuzichukua faida

hizo pasipo kutupilia mbali mambo yake ambayo yana faida pia kwani ‘kimfaacho mtu chake’.

Uhusiano baina ya tendo na tukio ni kanuni ya msingi katika maadili, ambapo wataalamu kama vile Baron & Goodwin (2020) wanasisitiza kuwa, kwa kila tendo, kuna tokeo ambalo linalandana na tendo hilo. Kwa msingi huu, Mwalimu analenga kuiasa jamii kufikiri kabla ya kutenda na dhima hiyo inalengwa na methali za Kiswahili kama zilivyojadiliwa katika kipengele hiki. Kwa jumla, tunaona wazi uhusiano baina ya hotuba za Mwalimu na semi za Kiswahili, ambavyo, vyote kwa pamoja, vinaonesha kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya tendo na tokeo.

**Nukuu zenye mwangwi wa semi zinazohusiana na uhuru**

Semi zina sifa ya kuamsha hisia fulani ndani ya mtu. Hisia hizo hujenga namna fulani ya kufikiri pamoja na kuathiri uneni na utendaji wa mtu huyo. Mathalani, usemi wa "Mwenye shibe hamjui mwenye njaa" huweza kuibua hisia ya uchungu au hasira kwa hadhira. Usemi huu humchochea kutambua hali yake. Pia, humwezesha kutambua kuwa hakuna atakayekuja kumsaidia, bali yeye mwenye kujua uchungu wa hali yake ndiye anawajibika kujipigania na kujitoa katika hali hiyo aliyomo.

Ziko nukuu kadhaa za Mwalimu ambazo zimebeba mtazamo huu, hasa anapozungumzia uhuru na maendeleo. Anasema: “*Freedom… it has to be won, and protected by those who desire it*” (Nyerere, 1973:3), ambapo anamaanisha kuwa, “Uhuru… unatakiwa kupiganiwa, na kulindwa na wale wanaoutamani”. Kauli hii inalandana na ile anayoitoa anapozungumzia masuala ya uhuru, umoja na ubaguzi wa rangi. Anasema:

> *And if I am humiliated merely for existing, then i have no alternative but to fight with whatever weapons are available. Yet this sort of fighting prevents us all, the man who discriminates as well as me from living a full life or contributing to human progress* (Nyerere, 1966:228).

> Na iwapo ninadhalilishwa kwa kuwapo tu, basi sina njia mbadala ila kupigana kwa silaha zozote zilizopo. Hata hivyo, namna hii ya kupigana hutuzuia wote, yule anayenibagua na mimi kuishi maisha kamili (yenye tija) ama kuchangia maendeleo ya mwanadamu.

Kupitia nukuu hizi mbili, tunabaini mambo yafuatayo: Kwanza, uhuru kilikuwa kitu cha msingi sana kilichomshughulisha Mwalimu na kuchukua sehemu kubwa ya fikra zake. Pili, uhuru lazima upatikane kwa kuudai kwa sababu mtu ambaye anamkandamiza mwenzake angependelea kuendelea na hali hiyo kwa sababu inamfaidisha. Tatu, katika kupigania uhuru, mtu huwajibika kutumia mbinu yoyote ili kufanikiwa. Mawazo haya yanadhihirika kupitia methali za Kiswahili kama vile, "Vita havina macho", "Amani haiji ila kwa ncha ya upanga" na nahau isemayo "Amsha timbwili".

Kupitia semi hizi, tunaona mambo kadhaa. Mosi, katika kupigana vita yoyote ile, mathalani vita ya uhuru, hakuna kuchagua mbinu na athari haichagui wa kumpata. Pili, ili amani iwepo, ni lazima watu wawe tayari kuipigania. Tatu, pasipo na amani, hapana uhuru. Nne, mtu anapokandamizwa kwa muda mrefu, hulazimika kupambana ili kujiweka huru. Hii ina maana kuwa, hata kama mtu huyu alilala kififikra au ana kiwango kikubwa cha uvumilivu, utafika wakati atafikia hatua ya kushindwa kuendelea kuvumilia, hivyo, kama Waswahili wasemavyo, atalazimika "kuamsha timbwili." Kwa jumla, Mwalimu aliona kuwa uhuru na maendeleo haviwezi kutenganishwa. Kwa mtazamo huu, kupokwa kwa

uhuru ni kupokwa kwa maendeleo na kukosekana kwa maendeleo hupelekea mtu kuwa tegemezi, hivyo, kupoteza uhuru wake.

**Nukuu zenye mwangwi wa semi zinazohusiana na umoja**

Kipengele hiki kinawasilisha na kujadili data za hotuba za Mwalimu kuhusu umoja, kama jambo mojawapo la msingi lililomshughulisha kwa sehemu kubwa. Kupitia kauli za Mwalimu, mtu anaweza kujifunza mambo mengi kuhusu dhana ya umoja kwa wanajamii. Kupitia hotuba zilizotafitiwa, ilibainika kuwa Mwalimu ana fikra nyingi kuhusu umoja.

Kwanza, Mwalimu aliamini kuwa Afrika ni moja na watu wake ni wamoja ingawa wana tofauti za kimaeneo na kitamaduni. Katika kubainisha mawazo yake juu ya hili, anasema: "*We in Africa are ONE, and we must remain so*" (Nyerere, 1966:161), yaani "*Sisi katika Afrika ni wamoja na inatupasa kubaki hivyo*". Katika nukuu hii, tunaona namna ambavyo hakulitazama suala la umoja kwa mawanda finyu ya kitaifa pekee, bali aliona kuwa Afrika, pamoja na tofauti zake, haina budi kubaki kuwa moja. Aidha, anaona kuwa umoja ndio nguzo ya nguvu na uwezo wa Afrika, na, kwamba, iwapo nguzo hii itaharibiwa, basi Afrika itakuwa dhaifu. Akisisitiza kuhusu athari za Afrika kutokuwa na umoja, anasema, "*The balkanization of Africa is a source of weakness to our continent*" (Nyerere, 1966:90). Nukuu hii inamaanisha, "Kugawanywa kwa Afrika (katika vieneo vidogo vyenye uadui) ndicho chanzo cha udhaifu kwa bara letu."

Katika fasihi ya Kiswahili, kuna semi mbalimbali zenye mawazo yanayolandana na mawazo ya Mwalimu juu ya umoja. Kwa mfano, kuna methali, "Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu" na "Nifae kwa mvua nikufae kwa jua." Methali hizi zinaashiria hali ya mtu mmoja na mwingine

au jamii moja na nyingine kuhitajiana. Katika kuhitajiana huku, watu na jamii yote hupata nguvu.

Kwa mujibu wa Mwalimu, kuwapo kwa Afrika kama jamii kunategemea kuwapo kwa umoja. Pia, uhuru wa Afrika unategemea umoja. Kwa maana hiyo, pasipo umoja, Afrika haiwezi kujitawala. Katika kuthibitisha hili, anasema, "*Only with unity can we be sure that Africa really governs Africa*" (Nyerere, 1966:190). Anamaanisha kuwa, "Ni kupitia umoja pekee tunaweza kuhakikisha kuwa Afrika inajitawala kwelikweli." Maudhui haya yanashabihiana na methali zinazosema "Kidole kimoja hakivunji chawa", "Kinga na kinga ndipo moto ukawaka." Kupitia semi hizi zilizorejelewa, tunaona kuwa, ili watu waweze kujikomboa na kujitawala kiuchumi, hawana budi kushirikiana.

Pili, anaikumbusha jamii kutambua kuwa, katika kujenga umoja kutofautiana hakuepukiki. Hivyo, ni muhimu kutarajia hayo na kutafuta namna bora ya kutatua tofauti wakati umoja ukiendelea kujengwa. Anasema:

> *Cooperation and conflict are two sides of the same coin; both arise out of man's relationship with his fellows. The larger the group, the greater the possibility of development through cooperation and the greater the possibility of conflict* (Nyerere, 1966:267).
> Ushirikiano na migogoro ni pande mbili za sarafu; yote hutokana na uhusiano wa mwanadamu na wenzake. Kadri kundi linavyokuwa kubwa, ndivyo uwezekano wa kupata maendeleo kama kundi unavyokuwa mkubwa vilevile ndivyo uwezekano wa kutofautiana unavyokuwa mkubwa.

Kauli hii ni angalizo kwa wale wenye nia ya kufikia maendeleo kwa njia ya ushirikiano. Anaamini kuwa njia ya kufikia maendeleo kwa urahisi na uharaka ni kushirikiana, ambapo kila mmoja katika kundi atachangia uwezo

na ujuzi alio nao kwa maendeleo ya wote. Hata hivyo, jambo hili linapofanyika, huwapasa wahusika kujiandaa kutatua mizozo inayoweza kuibuka.

Mawazo haya yanashadidiwa na methali isemayo, “Vikombe kabatini haviachi kugongana”, ikimaanisha kuwa, watu wanapoishi, pamoja hawakosi kupishana. Hivyo, jamii inatakiwa kuweka mikakati ya utatuzi, na, hivyo, umoja kuendelea pasipo kuvunjika.

Tatu, ili kufikia umoja wa kweli, ni vema kutambua kuwa wanadamu watakosea kwa kufanya mambo ya kuchukiza, kusikitisha au kukatisha tamaa. Hata hivyo, jambo hili lisiwe sababu ya kuvunjika kwa umoja. Inapotokea mmoja amekosea, basi asishambuliwe kwa sababu kufanya hivyo huwafaidisha wale wanaotaka umoja uvunjike. Mawazo haya yanadhihirika kupitia kauli ya Mwalimu anaposema, “*Our brothers may be wrong but they remain our brothers. This appears to me the only attitude open to us on our path to real unity*” (Nyerere, 1968:297). Kauli hii inamaanisha kuwa, “inawezekana ndugu zetu wakakosea, lakini wanabaki kuwa ndugu zetu. Huu ndio mtazamo pekee unaofaa katika njia yetu kuelekea umoja halisi”. Mawazo haya yanashabihiana na methali zinazosema, “Damu nzito kuliko maji” na “Ndugu humwui, afadhali kuwa naye”. Katika methali hizi, tunaona kuwa ndugu wanafaa kusameheana na kuwa kosa halivunji undugu. Methali hizi zinalenga kuijengea jamii hulka ya kusamehe kwa wepesi ili ushirikiano uendelee kuwapo kwa maendeleo ya wahusika.

Nne, maendeleo na umoja haviwezi kutenganishwa. Mwalimu aliamini kuwa kutofikiwa kwa umoja ndio kutofikiwa kwa maendeleo katika nyanja

zote. Haya yanadhihirika kupitia kauli yake anapojadili masuala yanayohusu uhusiano wa kimataifa. Anasema:

> *Thirty-six separate sticks of wood might each break under the weight of a heavy burden; but what if those thirty-six sticks of wood are bound together? Then the burden can be carried safely, and every single stick remain whole* (Nyerere, 1966:326).
>
> Vijiti thelathini na sita vilivyotengwa vinaweza kuvunjika kutokana na uzito wa mzigo, ila itatokea nini iwapo vitakuwa vimefungwa pamoja? Bila shaka mzigo utabebwa salama na kila kijiti kitabaki kikiwa kizima.

Katika kuonesha kuwa suala hili la umoja ni muhimu, analipa uzito katika akili yake. Mwalimu anasisitiza kwa kusema:

> *For each one of us is so weak in isolation that we compete with each other for the favour of the wealthy, and our separate but contiguous economies strain and weaken each other as they move in different direction at the same time* (Nyerere, 1966:336).
>
> Kila mmoja wetu ni dhaifu mno akiwa peke yake kiasi kwamba tunashindana wenyewe kwa wenyewe ili kupata upendeleo wa (mataifa) tajiri, na uchumi wetu unaotegemeana unaendelea kusongwa na kudhoofishana ukivutwa katika pande tofauti kwa wakati mmoja.

Mwalimu anatoa angalizo kuwa njia rahisi ya Afrika kutofikia maendeleo ni kwa kila nchi kujitenga na kufanya mambo yake pasipo ushirikiano. Anasema: "*Africa must travel together, as one, or no part of it will arrive to its destination*" (Nyerere, 1966:327), yaani "Ni lazima Afrika isafiri kama kitu kimoja, kama sivyo hakuna sehemu yake itakayofika salama."

Katika kauli hizi, Mwalimu anaonekana kuwa na mtazamo kuwa Afrika ni kitu kimoja ijapokuwa kuna mipaka ya kijiografia inayotenga taifa moja na jingine. Kwa sababu hiyo, maendeleo yake yanatarajia mchango wa kila taifa kwa pamoja; iwapo hili litashindikana, basi Afrika haiwezi kufikia

maendeleo yanayotarajiwa. Mtazamo huu unawasilishwa kupitia semi za Kiswahili kama vile “Jifya moja haliivishi chakula” na “Mkono mmoja hauchinji ng’ombe”. Kupitia methali hizi, tunatambua kuwa umoja ni amali ya msingi kwani uhai na usalama wa jamii hutegemea umoja wa jamii husika. Katika kuonesha umuhimu wa amali hii, jamii ya Waswahili ina methali zenye ukali kama vile, “Mkataa wengi mchawi” na “Sauti ya wengi ni sauti ya Mungu”. Methali hizi zinadhihirisha umuhimu wa suala la umoja katika jamii.

Tano, umoja haupatikani kwa maneno matupu. Mwalimu anaona kuwa lazima kuwe na nia ya kweli, mipango madhubuti pamoja na matendo ili kufikia umoja wa kweli. Anasema:

> *Psychologically we have been so successful that no African leader even if he does not believe such unity would dare say so. What is needed therefore is not more preaching about unity but more practicing of unity* (Nyerere, 1966:300).
>
> Kisaikolojia tumefanikiwa sana, kiasi kwamba hakuna kiongozi wa Afrika hata asiyeamini umoja wa namna hii anaweza kudiriki kukiri hilo. Kinachotakiwa sasa sio mahubiri zaidi kuhusu umoja, bali kuuweka umoja huo katika vitendo.

Kutokana na kauli hii, tunaweza kusema kwamba Mwalimu aliamini kuwa, “maneno matupu hayavunji mfupa”, “Maneno si mkuki” na “Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo”. Hii ni kusema kuwa, ni rahisi sana kutoa kauli nzito kuhusu jambo fulani. Hata hivyo, mtu hapaswi kuaminiwa wala kusifiwa kwa maneno matupu, bali kwa matendo yake. Vivyo hivyo, katika kuleta umoja, maneno matupu hayafai kitu, bali vitendo ndilo jambo linaloweza kuleta athari na kufikia lengo lililokusudiwa.

Katika hotuba aliyoitoa tarehe 6 Machi 1997 akiwa Accra, Ghana, anazungumzia mustakabali wa umoja wa Afrika katika karne ya 21. Mwalimu anaonesha kutokata tamaa juu ya umoja wa Afrika, ambapo anawausia viongozi waliopo kufanya kazi na kuwajibika kufikia umoja huo. Anasema:

> *So this is my plea to the new generation of African leaders and African peoples: work for unity with the firm conviction that without unity, there is no future for Africa. That is, of course, assuming that we still want to have a place under the sun.*[1]
>
> Kwa hiyo, hili ndilo ombi langu kwa kizazi kipya cha viongozi wa Afrika na watu wa Afrika. Fanyieni kazi umoja mkiwa na imani madhubuti kuwa pasipo umoja hakuna kesho ya Afrika. Hii ni iwapo tu bado tuna lengo la kuendelea kuishi.

Nukuu hii inaonesha kuwa kuwapo au kutokuwapo kwa Afrika kunategemea uamuzi wa viongozi wa Afrika juu ya suala la umoja. Jambo hili linaakisiwa na methali kama vile, "Kupanga ni kuchagua". Mpaka mwisho, Mwalimu anaendelea kuamini kuwa kuendelea kushikilia utengano wa mipaka ambayo Afrika ilirithi kutoka kwa wakoloni—kwa kung'ang'ania Utanzania, Ughana ama Ukenya na mambo ya aina hiyo—ni kuendelea kukumbatia fikra za ukoloni. Anaamini kuwa Afrika ni moja na inatakiwa kubaki hivyo.

Katika mjadala wa kipengele hiki, imebainika kuwa hotuba za Mwalimu juu ya umoja na mshikamano zinalandana na semi za Kiswahili. Hii inaonesha kuwa, utamaduni na amali za jamii, ikiwamo fasihi, huweza kuathiri mtu kwa kipindi chote cha maisha yake. Aidha, tumeona kuwa lengo hili

[1]Chanzo: https://newafricanmagazine.com/nyerere-without-unity-there-is-no-future-for-africa/

adhimu lilimshughulisha Mwalimu tangu mwanzoni mwa uongozi wake hata katika miaka ya mwisho ya uhai wake.

**Nukuu zenye mwangwi wa semi zinazohusiana na kuwajibika**

Kwa mujibu wa TUKI (2004), wajibu ni kitu au jambo ambalo mtu hutakiwa kufanya au kuamu—kama vile kazi, sharti, faradhi au jukumu. Sanaa, ikiwemo fasihi, kwa upana, na, semi, kwa umahsusi wake, huathiri namna ya mtu kufikiri kwa kumuumbia namna mpya ya kutazama watu, vitu, hali na maisha kwa jumla (Mack, 2011). Miongoni mwa athari ambazo hadhira hupata kutoka katika kazi za sanaa ni kumtafakarisha mwanadamu kuhusu wajibu wake katika maisha. Hii ina maana kuwa, mtu anaposikia semi fulani, udadisi kuhusu wajibu au jukumu lake huamshwa. Udadisi huo humfanya ajiulize maswali kama vile: "Je kuna namna mpya na bora ya kuishi zaidi ya hii ya sasa?" "Je, kuna uwezekano wa kujenga ulimwengu bora kuliko huu anaoishi sasa?" "Je, kuna tumaini la kujinasua kutoka alipo?" na "Je, ni kwa namna gani anaweza kufikia lengo hilo?"

Katika hotuba yake ya kuaga taifa kama rais mwaka 1985, mojawapo ya mambo ambayo Mwalimu aliyapa uzito ni umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii. Jambo hili hakulielekeza kwa wazawa pekee, bali alilielekeza pia kwa wageni ambao walikuwa wameingia Tanzania kama wakimbizi. Mwalimu aliamini kuwa, utu wa mtu na kufanya kazi ni mambo ambayo hayawezi kutenganishwa. Anasema:

> *We have implemented the Swahili proverb "mgeni kwa siku mbili, siku ya tatu mpe jembe". Some of the refugees have now become Tanzanian citizens, equal with all others and others have settled*

> *among us and are contributing to our production and development…*[2]
>
> Tumetekeleza methali ya Kiswahili, "Mgeni kwa siku mbili, siku ya tatu mpe jembe". Baadhi ya wakimbizi sasa wamekuwa raia wa Tanzania, sawasawa na wengine, na wako ambao wanakaa miongoni mwetu wakichangia katika uzalishaji wetu na maendeleo ..."

Kupitia nukuu hii, tunaona fikra za Mwalimu juu ya mtu, utu na dhana ya kazi. Kwake, utu wa mtu ulikamilika pale mtu huyo alipofanya kazi za kuchangia maendeleo ya jamii aliyomo. Mwalimu aliamini kuwa kila mtu, kwa hali na uwezo wake, ana wajibu wa kufanya kazi hata kama ni mgeni katika jamii fulani. Ili kufikisha ujumbe wake kwenye hotuba tajwa, Mwalimu anatumia methali ya Kiswahili inayoonesha kuwa, kwa Waswahili, mgeni hukirimiwa na kuachwa apumzike kwa siku chache. Baada ya muda, mgeni huyo hutarajiwa kufanya kazi akishirikiana na waliomkarimu.

Aidha, Mwalimu anaona kuwa kitendo cha mtu kutarajia kupokea msaada wakati yeye hana nia ya kuchangia chochote ni unyonyaji. Vilevile, anaashiria kuwa si kawaida kwa jamii ya Afrika kuwa na wanyonyaji wanaokaa tu katika jamii bila kufanya kazi huku wakitarajia kupata faida kutoka kwa wenzao. Mawazo haya yanadhihirika kupitia nukuu ifuatayo:

> *Not only was the capitalist or the landed exploiter unknown to traditional African society, but we did not have the other form of modern parasite–loiterer or idler who accepts the hospitality of society as his right but gives nothing in return* (Nyerere, 1966:165).
>
> Sio tu kuwa bepari au mnyonyaji mwenye ardhi hakujulikana kwa jamii asili ya Afrika, bali hatukuwa na aina yoyote ya

[2] Farewell speech by the President Mwalimu J.K Nyerere, at the Diamond Jubilee Hall Dar es Salaam; 4th November 1985 (pg. 8)

> mnyonyaji wa kisasa-mzururaji na mvivu ambaye hupokea ukarimu wa jamii kama haki yake pasipo yeye kutoa chochote.

Nukuu hii inaonesha jinsi jamii ya Afrika, ikiwamo Tanzania, ilivyothamini suala la kufanya kazi kama sehemu ya thamani ya mtu. Matarajio ya jamii hii ni kuwa kila mtu atatoa mchango wake kwa jamii kwa njia ya kufanya kazi. Matarajio haya yanadhihirika kupitia methali kama vile, "Mwenda bure si mkaa bure huenda akaokota", "Riziki ya mbwa iko miguuni mwake" na "Mgaagaa na upwa hali wali mkavu". Methali zingine za Kiswahili zinazosisitiza thamani ya kazi ni "Asiyefanya kazi asile", "Mkulima ni mmoja walaji ni wengi" na "Mzoea kutwaa, kutoa ni vita". Kupitia methali hizi, tunapata mambo kadhaa kuhusu kazi. Mosi, kufanya kazi ndio msingi wa maisha ya mtu kwani mtu hawezi kuishi bila kula, na, ili ale, anatakiwa kufanya kazi. Pili, katika jamii halisi, wako watu ambao wanapenda kula, lakini ni wavivu wa kuzalisha. Kwa ujumla, methali hizi zinamaanisha kuwa, katika jamii, haitarajiwi kuwa mtu atakaa bure pasipo kujishughulisha. Mtazamo huo unatokana na imani kuwa riziki haiji yenyewe na kumfuata mtu mahala alipokaa, bali inatakiwa kutafutwa kwa jitihada za makusudi.

Fikra nyingine inayojitokeza katika hotuba za Mwalimu kuhusu kazi ni kutokata tamaa. Kimsingi, changamoto katika kufanya kazi haziepukiki. Hivyo, mtu hutakiwa kujiandaa kukabiliana nazo kabla hazijatokea. Mwalimu anadhihirisha hoja hii kupitia nukuu inayosema:

> *When you have pushed the load a little way up a hill, it is no use relaxing. You have to go on. Otherwise, the load may well fall back to its original position and perhaps crush the people in the process* (Nyerere, 1968:169).

> Unapokuwa umesukuma mzigo umbali kiasi kwenye kilima, hakuna maana kupumzika. Lazima uendelee mbele. Tofauti na

> hapo, mzigo huweza kurudi nyuma pale ulipokuwa awali na pengine ukawaponda watu wakati wa kurudi chini.

Nukuu hii inaakisi nahau zisemazo, "Jifunge mkaja" na "Kaza buti" zikimaanisha 'fanya bidii' na 'usijihurumie'. Hii inamaanisha kuwa, mtu anapoanza kazi fulani, humpasa kupambana mpaka mwisho kwani kukata tamaa njiani huweza kusababisha hatari kubwa kuliko ilivyokuwa mwanzo.

Kwa upande mwingine, Mwalimu aliamini kuwa hakuna falsafa yoyote inaweza kufanikiwa bila watu kuamua kwa dhati kufanya kazi hata kama falsafa hiyo ni nzuri. Akizungumzia falsafa ya ujamaa kama ambavyo ilikuwa inafuatwa na Tanzania, anasema: "*There is no such a thing as socialism without work*" (Nyerere, 1966:165), yaani hakuna ujamaa pasipo kazi. Akisisitiza zaidi kuhusu wanaotegemea bahati katika kupata mafanikio, anasema, "*There is nothing good that can be had free of charge*" (Nyerere, 1966:58), yaani hakuna jambo jema linaloweza kupatikana bila malipo. Anachosisitiza hapa ni kuwa jambo lolote jema haliwezi kupatikana kinasibu tu pasipo kufanyiwa kazi.

Mawazo haya yanaakisi methali kama vile "Mla cha uchungu na tamu hakosi", "Mchumia juani hulia kivulini", na "Baada ya dhiki faraja". Hii inaonesha kuwa, katika mchakato wa kupata mafanikio, mtu huanza kukutana na mambo magumu. Ugumu huo huweza kuwa kikwazo kwa mtu. Hivyo, mtu huyo hatakiwa kufanya uamuzi wa, ama kuendelea mbele, au kuacha. Mawazo ya Mwalimu pamoja na methali hizi ni viashiria kuwa suala la mtu kufanikiwa au kukwama hutegemea uamuzi wake mwenyewe. Tunahitimisha hoja hii kwa kuyakinisha kuwa kuna muumano baina ya hotuba za Mwalimu na semi za Kiswahili kuhusu dhana ya kazi.

Katika mkazo mwingine kuhusu uwajibikaji, Mwalimu anaona kuwa njia pekee ya kupambana na matatizo ni kuwajibika. Anasema *"We cannot hope to solve our problems by pretending they do not exist*" (Nyerere, 1966:179), akimaanisha kuwa hatuwezi kutumaini kutatua matatizo yetu kwa kujifanya kuwa hayapo. Anaongeza:

> *There is no short cut, no easy solution which can be applied to the problems of developing our country. Slogans will not give our people more to eat; nor will blaming our failures on any other country or on any other group of our own people* (Nyerere, 1966:308).
>
> Hakuna njia ya mkato wala hakuna suluhisho rahisi ambalo tunaweza kulitumia kuendeleza nchi yetu. Kaulimbiu hazitawapatia watu wetu chakula zaidi. Vilevile, kulaumu nchi nyingine kwa kushindwa kwetu ama kundi lolote la watu wetu hakutawapatia watu wetu chakula.

Kutoka katika nukuu hizi, inaonesha waziwazi kuwa Mwalimu hakuamini katika maneno matupu, kulalamika na kukaa pasipo kuwajibika; badala yake, aliamini kuwa suluhisho la kupata maendeleo ya taifa ni kuwajibika. Mawazo haya ya Mwalimu ni mwangwi wa methali zisemazo, "Maneno matupu hayavunji mfupa" na "Kelele za chura hazimzuii tembo kunywa maji". Kwa mujibu wa methali hizi, iwapo mtu anachukia hali aliyomo na anataka kuibadilisha, basi anawajibika kufanya matendo ambayo yataleta mabadiliko anayoyatamani badala ya kuishia katika malalamiko.

Mawazo haya kuhusu uwajibikaji yanatuibulia mambo mawili: mtu kutambua wajibu alio nao na kuuthamini. Hii ina maana kuwa haitoshi tu mtu kutambua wajibu wake, bali inafaa aingie hatua ya pili ambayo ni kuutendea kazi. Mambo haya mawili yanapigiwa upatu na Mwalimu kwa kusema, "*For words without actions, simply lay us open to ridicule. Unfortunately, it is those who do not intend to follow their words with*

*actions who usually shout the loudest*" (Nyerere, 1968:299). Anamaanisha kuwa maneno bila matendo hutuweka katika nafasi ya kudhihakiwa. Isivyo bahati, wale wasiokusudia kuambatisha maneno na matendo yao ndio ambao, kwa kawaida, hupiga kelele zaidi. Hivyo, Mwalimu anaona kuwa ni lazima maneno ya mtu yaambatane na matendo, fikra zinazoakisiwa vema na methali isemayo, "Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo"; yaani mtu yeyote anaweza kusema maneno, lakini matendo ndiyo humtofautisha muungwana na asiyekuwa muungwana. Methali zingine za Kiswahili zinazoshadidia umuhimu wa vitendo ni "Maneno matupu hayavunji mfupa", "Maneno si mkuki", "Debe tupu haliachi kuvuma" na "Mwenye kelele hana neno". Methali hizi zinasisitiza kuwa thamani ya mtu haipimwi kwa maneno yake, bali kwa uwajibikaji wa vitendo. Hivyo, zinawang'ong'a na kuwazindua watu ambao hupenda kusema maneno mengi, lakini hawatendi. Kwa jumla, kuna hali ya kulandana baina ya fikra za Mwalimu na semi za Kiswahili kuhusu suala la uwajibikaji.

**Nukuu zenye mwangwi wa semi zinazohusiana na kujitegemea**

Semi hutawaliwa na sifa ya kutumia lugha ya picha ambayo hulazimisha hadhira kufikiri na kuhusianisha picha hiyo na mazingira halisi. Hii ina maana kuwa mtu aliyepokea semi hana budi kufikiri kwa makini huku akizingatia hali aliyomo na mazingira yanayomzunguka ili kufumbua picha husika na kupata maana yake. Hali hii ndiyo humfanya kutambua hali ambazo, hapo awali, asingezitambua iwapo usemi tajwa usingetumika. Tunaweza kusema kuwa semi hutumika kumwamsha au kumzindua mtu na kumfanya aone ulimwengu wake kwa uhalisi, kisha kutafuta mbinu za kuuboresha.

Kuhusu hili, Mwalimu anasema: "*For too long we in Africa and Tanzania as part of Africa have slept and allowed the rest of the world to walk around and over us*" (Nyerere, 1968:32), yaani "Kwa kipindi kirefu sisi, katika Afrika na Tanzania, kama sehemu ya Afrika, tumelala na kuruhusu ulimwengu kutuzunguka na kutukanyagakanyaga." Kauli hii inaashiria hali ya mtu kuchoshwa na hali aliyomo. Pia, inaashiria hali ya mtu kutoka katika usingizi wa muda mrefu. Zaidi, inaonesha hisia za mtu aliyejitambua na kuona sababu ya kujitegemea kwani hawezi kutegemea msaada wa wale wanaochangia hali aliyomo au wanaofaidika na hali hiyo.

Nahau kama vile, 'Fanya mtu si kitu", "Fanya mtu kiatu" na "Fanya mtu tambara la deki" zinalandana na nukuu za hotuba za Mwalimu, zikiwa na dhima ya kumwamsha mtu na kumwonesha hali halisi aliyomo. Mathalani, mtu anapoonewa na kukandamizwa kwa kipindi kirefu, anaweza kuizoea hali ile. Akitokea mtu akamwambia, "Unajua mtu fulani amekufanya wewe tambara la deki", mtu huyu atapata picha ya tambara la deki—ambalo hutumiwa kufuta uchafu, hukanyagwa bila kujali na mwisho linapoisha matumizi kutupwa. Kupitia picha kama hii, mtu huzinduka na kuiona hali yake katika uhalisi, jambo ambalo huweza kumfanya aanze kufikiri namna ya kujikomboa kwa kujitegemea.

Aidha, kila kundi la watu huwajibika kujitegemea katika kujikomboa na kujiweka huru, na, iwapo msaada utatokea, basi utakuja kuunga mkono jitihada ambazo tayari zimewekwa na wale wanaohitaji kujikomboa. Haya yanadhihirika kupitia Mwalimu anaposema, "*It is impossible for one people to free another people, or even defend the freedom of another people.*" (Nyerere, 1973:3), yaani "Haiwezekani kundi moja la watu kuweka huru kundi jingine, au hata kulinda uhuru wa kundi jingine." Katika kauli hii,

tunapata wazo kuwa yule mwenye hitaji anatakiwa kujitegemea katika kulishughulikia pasipo kutegemea watu wengine. Wazo hili ni mwangwi wa methali za Kiswahili kama vile, “Raha ya kaburi aijuaye maiti”, “Raha ya maiti aijuaye mwosha”, “Kilio huanza mfiwa ndipo wa mbali wakaingia”, na “Mwomba chumvi huombea chunguche.” Wazo la msingi linalobebwa na methali hizi ni kuwa mtu mwenye shida fulani ndiye mwenye uchungu; hivyo, mtu huyo anatakiwa kujipigania bila kutarajia msaada kutoka kwa mtu mwingine. Ijapokuwa Mwalimu aliamini katika ushirikiano wa watu na mataifa kuleta maendeleo, bado alitambua kuwa watu na mataifa hayo wanatakiwa kuwa tayari kujitegemea badala ya kutegemea hisani kutoka nje.

Kwa jumla, hotuba za Mwalimu zinaonekana kuwa mwangwi wa semi za Kiswahili katika suala la kujitegemea. Fasihi, zikiwamo semi, humwezesha mtu kutalii maisha yake, hali yake, mitazamo ya kilimwengu na kutoa nafasi ya kuhakiki maisha. Aidha, huweza kuathiri hisia za jamii na, wakati mwingine, kuamsha ari ya kujitegemea na kujikomboa.

**Nukuu zenye mwangwi wa semi zinazohusiana na malezi**

Suala la malezi ya watoto linachukua nafasi kubwa katika ujenzi wa jamii na taifa. Inatarajiwa kuwa malezi anayopata mtu katika makuzi yake yamtofautishe na mwingine ambaye amepata malezi ya aina tofauti. Hii ni kusema kuwa mtu mzima aliyeko katika jamii ni zao la malezi aliyopewa katika kipindi chote cha makuzi yake. Kwa sababu ya uzito huo, jamii ya Tanzania ina semi zinazoangazia suala hili. Wakati huohuo, suala hili limeshughulikiwa na Mwalimu katika hotuba zake. Uhusiano huu ndio unajadiliwa katika kipengele hiki.

Wazo mojawapo la Mwalimu kuhusu malezi ni kuwa msingi wa mtu hujengwa tangu anapokuwa mtoto. Hii ina maana kuwa msingi wa namna mtu anavyofikiri, anavyotazama ulimwengu na watu wanaomzunguka, pamoja na utambuzi wa maadili hujengwa tangu anapokuwa mtoto. Katika hili, Mwalimu anasema:

> *Our values in life were developed when we were young; the way we regard our fellows, the way we react to the right or wrong-all these things have developed from our childhood experiences at home and at school ... The real basis of the society of free individuals is the attitude of mind of the individuals who form the free society. And every knowledgeable person now agrees that attitudes of mind are shaped very largely when a person is very young* (27/8/1966[3]).
>
> Maadili yetu katika maisha yalijengwa tulipokuwa wadogo, namna tunavyowachukulia wenzetu, namna tunavyoitikia mema na mabaya—haya yote yamejengwa kutoka katika uzoefu tulioupata katika utoto tukiwa nyumbani na shuleni … Msingi wa kweli wa jamii ya watu huru ni mtazamo wa fikra za watu wanaounda jamii huru. Na kila mtu mwenye uelewa sasa anakubali kuwa mitazamo ya fikra hujengwa, kwa kiasi kikubwa, mtu anapokuwa bado mdogo sana.

Kutokana na kauli hizi, tunauona mtazamo wa Mwalimu juu ya malezi ya watoto na namna ambavyo malezi hayo yanaweza kuathiri mtu mmojammoja au jamii.

Nukuu za hotuba za Mwalimu kuhusu malezi zinaakisi semi za Kiswahili kama vile, “Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo”, “Samaki mkunje angali mbichi”, “Rada ya mwana ufito’ na “Mchelea mwana kulia hulia yeye.” Methali zote hizi zinabeba fikra kuwa malezi ni suala la msingi na linatakiwa kuwekewa msisitizo na jamii. Aidha, methali hizi zinaelekeza kwamba, katika jamii, suala la malezi si la wazazi pekee, bali ni jukumu la

[3] “The power of teachers” Hotuba iliyotolewa na Mwalimu Chuo cha Ualimu Morogoro tarehe 27 Agosti 1966

walimu na wanajamii wote. Hapo ndipo Waswahili husema, "Mkono mmoja haulei mwana" wakimaanisha kuwa kazi ya malezi ya watoto haitakiwi kuachwa kwa mtu mmoja au kundi moja la watu (kama vile wazazi au walimu). Kwa kuwa hili ni jukumu la msingi katika ujenzi wa jamii bora, basi linatakiwa kufanywa na jamii yote iwapo jamii hiyo inatarajia kuvuna matokeo chanya.

Wazo jingine kuhusu malezi tunalolipata kutoka kwa Mwalimu ni kuwa matendo ya watu wazima katika jamii yanaweka msingi wa kizazi kijacho kwani wale ambao ni wadogo wanajifunza kutoka kwa watu wazima. Kuhusu hili, anasema, "*Our actions are forming the traditions of the future; what we do and how we react to external events will set a pattern which our descendants may find difficult to break*" (Nyerere, 1966:252), yaani "Matendo yetu yanajenga desturi za wakati ujao, tunalofanya sasa na namna tunavyoitikia matukio ya nje vitaweka mfumo ambao vizazi vyetu vinaweza kushindwa kuuvunja."

Mwalimu anatoa angalizo kwa viongozi na jamii yote kuwa matendo yao ya sasa yana athari kwa vizazi vinavyofuata kwani vinaweza kupata ugumu kuvunja mfumo ambao tayari umejengeka na kukubaliwa katika jamii kama desturi inayotakiwa kuzingatiwa. Katika angalizo hili, tunaona nahau kama vile "Jenga tabia" ikiakisiwa, kwa maana kuwa tabia haitokei ghafla, bali hutokea kwa kurudia tendo fulani mara kwa mara. Kwa upande mwingine, methali kama "Usipoziba ufa, utajenga ukuta" hubeba mtazamo huohuo ikimaanisha kuwa, ili tendo lisilete madhara makubwa, linatakiwa kushughulikiwa mapema. Vivyo hivyo, katika malezi, semi hizi zinaasa kuwa huwapasa watu wazima kujihadhari na matendo ambayo yanaweza kujenga desturi hasi iwapo yataachwa kuendelea. Hii inaonesha kuwa,

katika malezi, jamii ina wajibu wa kupanda mbegu nzuri kwa watoto na inawajibika kuhakikisha kuwa inaakisi mbegu hiyo kwa matendo yake.

## Hitimisho

Katika makala hii, imebainishwa namna ambavyo nukuu za hotuba za mwalimu zimekuwa mwangwi wa semi za Kiswahili. Kiini cha mjadala kimeshikiliwa na vipengele sita ambavyo vinachimbuka kutoka kwenye maudhui yaliyobeba uzito katika hotuba za Mwalimu zilizotafitiwa. Vipengele hivyo ni uhusiano kati ya tendo na tokeo, uhuru, umoja, uwajibikaji, kujitegemea, na malezi. Katika mjadala huu, imedhihirika kuwa nukuu za hotuba za Mwalimu zinaakisi semi za Kiswahili na fikra za jamii ya Tanzania kuhusu vipengele vilivyotajwa. Katika nukuu zilizorejelewa, kuna vipengele ambavyo mbinu ya mwangwi imetumiwa kwa makusudi, ambapo Mwalimu amerejelea semi mbalimbali za Kiswahili katika hotuba zake. Pia, kuna maeneo ambayo imefanyika kwa njia isiyokuwa ya wazi. Kwa jumla, kupitia hotuba za Mwalimu uhusiano baina ya fikra za Mwalimu na semi za Kiswahili umedhirika. Uhusiano huu unadhihirisha hoja kuwa fasihi ni taaluma mtambuko ambayo inagusa nyanja mbalimbali za maisha. Kwa sababu hiyo, ni muhimu uga wa fasihi usifundishwe na kutafitiwa kipwekepweke, bali kwa kuhusianishwa na nyuga zingine zinazogusa maisha.

## Marejeleo

Akida, H.H. (1981). Vitendawili na Methali. In C.K. Omari & M. Mvungi (Eds.), *Urithi wa Utamaduni Wetu* (kur. 89-111). Dar es Salaam: TPH.

Alfarhan, E.A. (2024). The Influence of Literature on the Society. *International Journal of Social Science and Humanities Research*. 12(1), 263-270.

Albrecht, M.C. (1954). The Relationship of Literature and Society. *American Journal of Sociology*. 59(5), 425-436.

Anderson, S.L. (2017). *Echo and Meaning on Early Modern English Stages*. Germany: Springer International Publishing.

Baron, J. & Goodwin, G.P. (2020). Consequences, Norms, and Inaction: A Critical Analysis. In *Judgment and Decision Making*. 15(3), pp. 421-442.

Bukenya, A.S., Gachanja, M., & Nandwa, J. (1997). *Oral Literature*. Nairobi: Longhorn Publisher.

Colby, E. (1920). *The Echo-device in Literature*. New York: New York Public Library.

Corcoran, P. (2001). Black Narcissus: Reflections on Identity in African Narrative. In L. Spaas & T. Selous (Eds.), *Echoes of Narcissus* (pp. 235-244). New York: Oxford: Berghahn Books.

Douglas, M. (2014). *Risk and Blame: Essays in Cultural Theory*. London: Routledge.

Hoggart, R. (1970). *Speaking to Each Other: About Literature*. London: Chatto and Windus Publications.

Hoggart, R. (1998). *The Uses of Literacy*. Harmondsworth: Penguin Publications.

Hollander, J. (1981). *The Figure of Echo: A Mode of Allusion in Milton and After*. Berkeley: University of California Press.

Juliusnyerere.org. (2009). Hotuba ya Nyerere aliyoitoa tarehe 4 Novemba 1985 katika Ukumbi wa Diamond Jubilee. Inapatikana katika https://www.juliusnyerere.org/resources/view/farewell_speech_by_the_president_mwalimu_julius_k._nyerere_nov._1985.

Kavitha, K. (2023). Cultural Theory and Literature: Critical Analysis in Popular Fiction. *International Journal of Creative Research Thoughts*. 11(9), 818-825.

Keerthika, S. (2018). Literature and Society: How Literature Reflects Society. In *International Journal of Science, Engineering and Management*. 3(4), 471-472.

Mack, M. (2011). *How Literature Changes the Way We Think*. London: Bloomsbury Publishing.

Mng'aruthi, T.K. (2008). *Fasihi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: Kauttu.

Ndungo, M.C., & Wafula, R.M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi.

New African (2013). Hotuba ya Nyerere aliyoitoa tarehe 6 Machi 1997 jijini Accra: "Without unity, there is no future for Africa". Inapatikana katika https://newafricanmagazine.com/nyerere-without-unity-there-is-no-future-for-africa/

Nyerere, J.K. (1966a). "The Power of Teachers", Speech Given at the Morogoro Teachers' College, 27th August 1966.

Nyerere, J.K. (1966b). *Freedom and Unity: Uhuru na Umoja: A Selection from Writings and Speeches 1952-65 by Julius Kambarage Nyerere*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (1968). *Freedom and Socialism. A Selection from Writings and Speeches 1965-1967*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Nyerere, J.K. (1973). *Freedom and Development/Uhuru na Maendeleo: A Selection from Writings and Speeches 1968-1973*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Offermans, A. (2010). *History of Cultural Theory: A Summary of Historical Developments Regarding Cultural Theory*. Maastricht: ICIS.

Oswell, D. (2010). *Cultural Theory*. London: SAGE Publications Ltd.

Payne, M. & Barbera, J.R. (2010). *A Dictionary of Cultural and Critical Theory*. New Jersey: John Wiley & Sons, Inc.

Petrino, E. (2010). Allusion, Echo, and Literary Influence in Emily Dickinson. *The Emily Dickinson Journal.* 19 (1), 80-102.

Ryan, M. (2011). *The Encyclopedia of Literary and Cultural Theory*. New Jersey: John Wiley & Sons, Inc.

TUKI 2004. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, K.W. (2001). *Kamusi ya Methali*. Nairobi: Longhorn Publisher.

Williams, R. (1963). *Culture and Society*. Harmondsworth: Penguin.

Williams, R. (2006). The analysis of culture. In Storey. J (Ed.), *Cultural Theory and Popular Culture: A Reader* (pp. 32-40). Harlow: Pearson Education.